

## **BARAZA JIPYA LA WAFANYAKAZI WA TUME YA UTUMISHI WA UMMA KUZINDULIWA**

Tume ya Utumishi wa Umma ipo katika mchakato wa kuunda Baraza jipya la Wafanyakazi baada ya Baraza la zamani ambalo liliundwa Septemba, 2005 kumaliza muda wake 14/5/2008 kwa mujibu wa Katiba ya uwakilishi wa Mabaraza ya Wafanyakazi nchini

Kwa mujibu wa Katiba ya Baraza la Wafanyakazi, iwapo Baraza litavunjwa baada ya kumaliza muda wake, Baraza jipya linapaswa kuundwa katika sehemu husika ya kazi ili kutoa fursa kwa watumishi kupata uwakilishi. Kwa mantiki hiyo, tarehe 12/2/2009 Tume ya Utumishi wa Umma, Makao Makao Makuu Dar Es Salaam ilifanya mkutano ili kuchagua wajumbe wa baraza lake.

Katika uchaguzi huo wajumbe 26 wamechaguliwa kutoka katika Idara na Vitengo vya Tume ya Utumishi wa Umma Makao Mkuu. Aidha mchakato wa kuchagua wajumbe wa Baraza katika Mikoa ya Tanzania Bara uko katika hatua za kukamilishwa ili kupata wajumbe wengine 21 ambapo majina 11 kati ya wajumbe hao yamewasilshwa Makao Makuu. Wajumbe wengine 10 wa Halamashauri ya Tawi la TUGHE Makao Makuu Tume ya Utumishi wa Umma wanaendelea kuwa katika baraza jipya mpaka muda wao utakapomalizika. Aidha mwakilishi wa TUGHE kutoka Mkoa anaendelea kuwa mjumbe kwa

wadhifa wake na mwakilishi wa baraza kuu la wafanyakazi serikalini atayechaguliwa atakuwa mjumbe katika baraza jipya

Katika uchaguzi uliomalizika Jana katika ukumbi wa Karimjee Jijini Dar Es Salaam, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma ambaye amekuwa Mwenyekiti wa Baraza kwa Mujibu wa wadhifa wake, Bibi Tecla W. Shangali amewaahadi wajumbe waliochaguliwa kuwa Baraza jipya litazinduliwa mara baada ya Tume Makao Mkuu kupata majina ya wajumbe wote waliochaguliwa kutoka Mikoani. Lakini uzinduzi huo utatanguliwa na uchaguzi wa Katibu wa Baraza na msaidizi wake ambao watachaguliwa na wajumbe wote wa Baraza la Wafanyakazi.

Kwa mujibu wa Mkataba wa Baraza la wafanyakazi, Baraza litakuwa na majukumu ya kuishauri Serikali juu ya ufanisi wa kazi na hatua zinazofaa kuchukuliwa ili kuhakikisha kuwa huduma zitolewazo na wafanyakazi zinaridhisha na zimo katika lengo la Taifa, kuishauri Serikali juu ya mambo mengine yaanayohusu maslahi na hali ya wafanyakazi, kuishauri Serikali juu ya mabadiliko ya kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, masharti ya kazi na miundo ya utumishi, kushauri juu ya utaratibu wa kupandishwa vyeo wafanyakazi na nidhamu, kuwashirikisha wafanyakazi wa serikali katika utekelezaji wa shughuli za serikali kwa ushirikiano na uongozi

na kupkea na kuthibitisha mipango na makisio ya mapato na matumizi ya Tume ya Utumishi wa Umma.

Aidha Baraza na litajadili na kutoa ushauri kuhusu mipango ya Elimu kwa wafanyakazi kwa ujumla na elimu ya ujuzi, kujadili na kutoa ushauri katika matumizi ya ya fedha kufuatana na mgao unaotolewa na mamlaka husika

Baraza la wafanyakazi litafanya kazi kwa muda wa mika 3 na baada ya hapo litavunjwa na kuundwa baraza lingine jipya.